**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
**SHULE YA SEKONDARI AZANIA**

Simu: +255 688 060 825

Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz
headmaster@azaniasecondary.sc.tz

Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
S. L. P 9074,
Dar es salaam.
Upanga Magharibi.

---

Kumb. Na. DCC/AZSS/**F5**/____________

Tarehe **15** Juni **2024**

**KWA MZAZI / MLEZI WA --------------------------------**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI AZANIA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM KIDATO CHA TANO HADI CHA SITA MWAKA 2024/2025**

**1. UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao **AMECHAGULIWA /AMEHAMISHIWA** Shule ya Sekondari Azania kidato cha Tano/Sita mwaka **2024** Tahasusi ya **ECAc** [ ], **EGM** [ ], **PCB** [ ], **EBuAc** [ ], **PMCs** [ ], **(BuAcM)** [ ] na **PCM** [ ] .Shule ya Sekondari Azania ni ya **BWENI kwa kidato cha Tano na cha Sita tu. HONGERA NA KARIBU SANA.**

**2. MAHALI SHULE ILIPO:**

Shule hii ipo katika Barabara ya Umoja wa Mataifa karibu na kituo cha **ZIMAMOTO** (**FIRE**) **KATI YA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JANGWANI NA** Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

**3. MUHIMU**

Muhula wa masomo unaanza _____________, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe ____________. Mwisho wa kuripoti mwanafunzi ni tarehe ___________ baada ya tarehe hiyo **HATAPOKELEWA. Tunawakumbusha wazazi/walezi wa wanafunzi wa bweni kuwapa Watoto wenu kitambulisho cha Bima ya afya.**

**4. MAHITAJI YA SHULE.**

**(i )** Sare ya shule ni **Suruali ya rangi ya "Dark Green"(SIZE INCH 17 CHINI)** na **Shati jeupe la mikono mifupi (tomato) na Tai yenye rangi ya suruali**. Unatakiwa kuwa na jozi mbili za Suruali ambazo **ZITAPATIKANA HAPA SHULENI TU.**

**(ii)Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka**,Vyenye kisigino kifupi,vya Kamba na siyo raba.

**(iii) Soksi nyeusi** jozi mbili

(iv) **Mkanda mweusi** wa ngozi wenye kichuma cha kawaida cha Kufungia suruali.
(v) **Sweta moja** lenye rangi ya Suruali(kwa anayetaka).
(vi) **Sare ya michezo :** track suit na bukta bluu bahari.

5. **RATIBA YA SHULE huanza Saa 1.00 asubuhi** hadi **saa 8.30 mchana**.

**NB:** **RATIBA YA SIKU ZA IJUMAA huanza saa 1.00 asubuhi** na kuishia **saa 6.00 mchana** ili kuwawezesha **Wanafunzi wa Kiislamu** kuhudhuria **SWALA YA IJUMAA.** Pia Lugha ya mazungumzo awapo mazingira ya shule ni **KIINGEREZA.**

**6. KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**:

**A. MAHUDHURIO:**

Mwanafunzi hana budi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo Darasani na siku za masomo kwa mwaka (siku 194) . Mwanafunzi atakayeshindwa kuhudhuria **MBILI YA TATU (2/3**) ya siku hizo **BILA SABABU MAALUMU** atakuwa **AMEJIONDOA** mwenyewe shuleni.

**B. 1. MAHITAJI KWA WANAFUNZI WA BWENI:**

(i) Godoro la futi 2 ½ x 6 (lenye kitambaa)
(ii) Shuka mbili (2) futi 4 x 6 (light blue)
(iii) Chandarua futi 4 x 6 (cheupe)
(iv) Taulo na sanduku la bati (kuhifadhia nguo)
(v) Nguo za Kushindia ni T-shirt 2 na suruali ambazo zitavaliwa muda wote awapo Bwenini (**Zinapatikana kwa malipo hapa shuleni). Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani. Nguo atakayokuwa ameivaa siku ya kuja shuleni, hataruhusiwa tena kuivaa muda wake wote wa kuwa hapa shuleni.**

**2. VIFAA VYA CHAKULA:**

(i) Sahani.
(ii) Kijiko.
(iii) Bakuli na Kikombe cha ½ lita.

**3. VIFAA VYA USAFI:**

(i) Ndoo ndogo mbili(2) za lita 10 (Plastiki)
(ii) Vifaa vingine vyote muhimu mfano: Sabuni za kuogea na kufulia za Kutosha, Mswaki, Dawa ya Meno n.k.

**"ANGALIZO":** Ni **marufuku** kwa mwanafunzi kuja na vitu vya thamani / hatarishi kama **Redio, TV, Laptop, Simu, kisu,** n.k. Ikitokea amekuja navyo basi amkabidhi mtu aliye msindikiza ili arudi navyo kwani akikamatwa na vitu hivyo bwenini atakuwa amevunja sheria.

**C. MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI:**

(i) Madaftari makubwa Matano (**Counter Books**)
(ii) Mathematics Set, **Scientific Calculator** na Four figure.
(iii) Kalamu za Wino na Penseli za kutosha.
(iv) Rula na kifutio.
(v) Rimu **A4** mbili za karatasi.
(vi) Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika (pata ushauri toka kwa mwalimu/Idara husika), mfano somo la Biology;

- **Biological science 3rd Ed. 2011 by D. J. Tayler N.P.O. Green and G.W. Staut**
- **Guide to dissection by HGQ Rowett, M.A., and M. I. Biology.**

**Dissection Kit** Kwa wanafunzi wa Somo la **Biology**.

**Geography :** Practical Geography for Advanced Secondary Schools na Physical Geography for Advanced Secondary Schools

(vii) Begi jeusi la kubebea vifaa vyake.

**NB: Vifaa vya usafi**

**EGM:** Chelewa -02 (zenye mti), Soft broom )- 02, Reki -01, Mopa na ndoo yake -01

**PCB:** Dust bins -01, Soft Broom 02

**PCM:** Chelewa 02 (zenye mti), Soft broom 02, Dawa ya kusafishia choo (ARO) - 01 na Hard broom 01

**ECAc :** Chelewa 02 (zenye mti), Soft broom ) 02, Sabuni ya Maji Dumu -01 la lita (5) - (FOMA/JET) na Squezer -01

**EBuAC**: Chelewa -02 (zenye mti), Hard broom 01, Squezer 01, Mkasi wa kukatia maua 01

**PMCs**: Chelewa 02 (zenye mti), Soft broom 02, Dawa ya kusafishia choo dumu 01 la lita (5) na Hard broom 01

**BuAcM:** Chelewa 02 (zenye mti), Soft broom) 02, Dawa ya kusafishia choo (ARO) - 01 na Squezer 01

Mwanafunzi azingatie usafi wake binafsi na mazingira ya shule kama vile mahali pa kulala (bwenini), vyoo, madarasa na maeneo yote yanayo zunguka shule.

**Ukumbi wa chakula**

**(i).** Mwanafunzi anatakiwa kula chakula katika ukumbi wa shule na si sehemu nyingine yoyote.
(ii). Mwanafunzi atalazimika kufanya usafi siku ya zamu yake katika ukumbi wa chakula na maeneo ya ukumbi.
(iii). Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za heshima anapoingia kwenye ukumbi wa chakula, ni marufuku kuingia na taulo, mswaki, bukta n.k.

**Bwenini**

**(i).** Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi wa kila siku katika eneo atakalo pangiwa na kiongozi wake.
(ii). Mwanafunzi lazima awepo kwenye ukaguzi wa siku ya usafi.
(iii).Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote katika mabweni wakati wote.
(iv).Ni marufuku kupeleka viti, meza na chakula bwenini.

## 7. MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE

.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**NB:** Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya Shule Na. **0150251317200** katika benki ya **CRDB.** Jina la akaunti ni **AZANIA SECONDARY SCHOOL** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi na Tahasusi yake( combination) kwenye risiti ya malipo ya bank.Isipokuwa Michango ya NEMBO na KITAMBULISHO ilipwe Shuleni.Unakumbushwa kuja na risiti ya malipo.

## 8.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais -Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.Mambo hayo ni pamoja na;

### 8.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**8.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 9. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**NB** **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0688 060 825 784 666 252**

**NAKALA KWA:**

: **Afisa elimu Jiji la Dar es Salaam.**
: **Afisa Elimu wa Mkoa.**
: **Mkaguzi Mkuu – Kanda ya Dar es salaam.**

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
**SHULE YA SEKONDARI AZANIA**

Simu: +255 688 060 825

Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz

headmaster@azaniasecondary.sc.tz

Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule,

S.L.P 9074,

Dar es salaam.

Upanga Magharibi

---

Kumb. Na. AZ/F5/____________
Tarehe …………

PICHA YA MWANAFUNZI

**YAH: FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)**
**SEHEMU "A" IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE.**
Jina kamili la Mwanafunzi ______________________________________
Tarehe ya kuzaliwa….../…..../…......(3) Mahali (Wilaya) __________________
(4) Uraia _____________________ (5) Dini__________Dhehebu__________
(6) Shule ya Msingi uliyosoma_______________________________________
Namba ya Mtihani PS. _______________________________________
(7) Shule ya Sekondari uliyopangwa (FI - IV) ___________________________
(8) Shule ya sekondari uliyotoka (FV) _________________________________
Nambari ya Mtihani S._________________________________________
(9) Mahali unapoishi kwa sasa ______________________________________

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

Mimi _________________________________ Nakubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha **Tano / Sita.**

Naahidi kutii kikamilifu Sheria / Kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa **AZANIA.**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI______________________TAREHE_______**

**SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI / MLEZI:**

PICHA YA MZAZI / MLEZI

1. Jina la Mzazi/Mlezi __________________________
2. Kazi ______________________________________
3. Anuani ____________________________________
4. Simu ______________________________________
5. Mahali ninapoishi_____________________________

**AHADI YA MZAZI / MLEZI YA KULIPA MICHANGO YA SHULE:**

Mimi______________________________Mzazi /Mlezi wa ____________________________ wa **Kidato cha tano/sita mwaka 20_____** katika **Shule ya sekondari AZANIA**. Nathibitisha na kuahidi kuwa nipo tayari kulipa **MICHANGO MBALIMBALI** kwa mwaka pamoja na michango mingine inayoidhinishwa na shule au mamlaka ya elimu kwa ajili ya maendeleo ya shule na wanafunzi.

Pia naahidi kuwa kila ifikapo mwisho wa **Muhula wa Shule** (**Mwezi Juni** au **Desemba**) Nitakuwa nimemaliza deni kwa mwaka huo. **Michango** italipwa na;

**SAINI YA MZAZI/ MLEZI_______________________________________ TAREHE_________**

**Jina la mjumbe (shina)___________________________ simu_________________________**

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
**SHULE YA SEKONDARI AZANIA**

Simu: +255 688 060 825
Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz
headmaster@azaniasecondary.sc.tz
Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule, S.L.P 9074,
Dar es salaam.

Upanga Magharibi

---

Kumb. Na. AZ/F5/________
Tarehe …………….

**FOMU NA 2: FOMU YA TAARIFA YA AFYA YA MWANAFUNZI "MEDICAL EXAMINATION FORM"**

**Maelezo**: Fomu hii ijazwe na Mganga Mkuu wa Mkoa /Wilaya / Kituo cha Afya na Mwanafunzi aje nayo shuleni na kuikabidhi ofisi ya nyaraka za wanafunzi.

Nathibitisha kuwa Mwanafunzi [Jina la mwanafunzi]_________________________
Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana anayo / hanayo afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;-

[A] **Hali ya mwili**

[I] Mapigo ya moyo ________________________________________
[ii] Haemoglobin;________________________________________
[iii] Kundi la damu [blood group]______________________________
[iii] Mkojo (Urine) ________________________________________
[iv] Kinyesi (Stool) ________________________________________
[vi] Macho yana kasoro ____________________________________
[vii] Masikio yana kasoro ___________________________________

**Angalia**: Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (**i**)-(**vii**)

[B] **Magonjwa**

[a]Bronchial asthma ________________________________________
[b] Tuberculosis ________________________________________
[c] Epilepsy ________________________________________
[d] Blood pressure ________________________________________
[e] Peptic/duodenal ulcers ________________________________
[f] Sickle cells ________________________________________
[g] Leprosy ________________________________________
[h] Venereal disease [give type] ____________________________
[I] Mental illness ________________________________________
[j] Any other serious disease not mentioned above

Jina na Saini ya Daktari………………………………………….. tarehe …………. Muhuri

**MUHIMU:**

Taarifa iliyothibitishwa na daktari ndiyo itakayofuatwa na shule na si vinginevyo.